# MAMLAKA YA MAENDELEO YA BIASHARA TANZANIA

TANZANIA TRADE DEVELOPMENT AUTHORITY

***Uchambuzi wa Bei za Bidhaa kwa Masoko ya Mkoa wa Dar es Salaam, Aprili, 2024.***

## 1. UTANGULIZI

Uchambuzi wa bei za jumla za bidhaa mbalimbali za *Kilimo, Viwanda na Mifugo* katika masoko ya Dar es Salaam kwa kipindi cha tarehe **21-27/04/2024** hadi **28/4/05 /2024 kwa bidhaa zinazouzwa katika ujazo mbalimbali** ni kama inavyoonekana kwenye jedwali lifuatalo:-.

## 2. UCHAMBUZI

| ***Mbogamboga*** | **KIASI** | **21-27/04/2024** | **28/4-4/05 /2024** | **Badiliko (%)** |
|---|---|---|---|---|
| Bamia | 50 KG | 47,500 | 40,750 | -14.21 |
| Bilinganya | 90/100 KG | 130,000 | 150,000 | 15.38 |
| Pilipili Hoho | 100 KG | 82,500 | 105,000 | 27.27 |
| Vitunguu Maji | >100 KG | 297,500 | 390,000 | 31.09 |
| ***Matunda*** | **KIASI** | **21-27/04/2024** | **28/4-4/05 /2024** | **Badiliko (%)** |
| Parachichi | 100KG | 32,500 | 45,000 | 38.46 |
| Passion | >100KG | 80,000 | 80,000 | 0.00 |
| ***Bidhaa za Mizizi*** | **KIASI** | **21-27/04/2024** | **28/4-4/05 /2024** | **Badiliko (%)** |
| Viaz vitamu | >1OO KG | 82,500 | 68,750 | 16.67 |
| Muhogo | KILOBA | 115,000 | 115,000 | 0.00 |
| Magimbi | 100KG | 222,500 | 222,500 | 0.00 |
| ***Viungo*** | **KIASI** | **21-27/04/2024** | **28/4-4/05 /2024** | **Badiliko (%)** |
| Mdalasin | 100KG | 150,000 | 150,000 | 0 |
| Tangawizi | 100KG | 137,500 | 137,500 | 0 |
| Pilipili Mbuzi | 100KG | 95,000 | 95,000 | 0 |
| ***Nafaka na Kunde*** | **KIASI** | **21-27/04/2024** | **28/4-4/05 /2024** | **Badiliko (%)** |
| Kunde | 100KG | 181,666 | 212,500 | (16.97) |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Maharage Mekundu | 100KG | 270,000 | 216,680 | 19.75 |
| Maharage Kombati | 100KG | 308,333 | 315,000 | (2.16) |
| Mahindi | 100KG | 68,000 | 82,500 | (21.32) |
| Mtama | 100KG | 108,750 | 140,000 | (28.74) |
| Unga Sembe | 100KG | 145,000 | 100,500 | 30.69 |
| ***Bidhaa za Uvuvi*** | **KIASI** | **21-27/04/2024** | **28/4-4/05 /2024** | **Badiliko (%)** |
| Dagaa wa Mwanza | 100KG | 825,000 | 800,000 | 3.03 |
| Dagaa wa Nyama | 100KG | 110,000 | 111,000 | 0.91 |
| Sato | 100 KG | 1,100,000 | 1,000,500 | 4.55 |
| Sangara | 100 KG | 900,000 | 900,000 | 0.00 |
| ***Bidhaa za Mifugo*** | **KIASI** | **21-27/04/2024** | **28/4-4/05 /2024** | **Badiliko (%)** |
| Kuku Kienyeji | MOJA | 20,000 | 22,500 | (12.50) |
| Kuku Kisasa | MOJA | 6,900 | 6,900 | 0 |
| Mayai Kienyeji | 1 TRAYI | 14,500 | 11,850 | 18.28 |
| Mayai Kisasa | 1 TRAYI | 10,500 | 9,750 | 7.14 |

| ***Bidhaa za Ujenzi*** | **KIASI** | **21-27/04/2024** | **28/4-4/05 /2024** | **Badiliko (%)** |
|---|---|---|---|---|
| Saruji 32.5 | 50KG | 16,250 | 16,250 | |
| Saruji 42.5 | 50KG | 17,500 | 17,500 | |
| Bati Geji 28 | Mita 3 | 36,000 | 36,000 | |
| Bati Geji 30 | Mita 3 | 21,000 | 21,000 | |

**Ufafanuzi wa bidhaa mbalimbali**

**Bidhaa za Mbogamboga**

Bei za bidhaa vitunguu maji zimeonekana kupanda zaidi kuliko bidhaa nyingine kwa wastani wa ailimia 31.09% kutoaka na kuongezeka kwa mahitaji na kushukwa kwa

uzalishaji wa bidhaa hiyo huku bei ya Bamia ikishuka zaidi kuliko bidhaa nyingine kwa wastani wa 14.21% katika kipindi hicho kutoaka na kuongezeka kwa maeneo ya uzalishaji wa bidhaa hiyo.

**Bidhaa za Matunda**

Bei ya Parachichi ilipanda kwa wastani wa asilimia 25% kutokana na kuharibika kwa miundo mbuinu ya usafirishaji wa bidhaa hiyo kutoka mikoa inayozalisha kama Tanga, Njombe na Mbeya huku bei ya Pasheni ikisalia hivyo hivyo katika kipindi chote hicho.

**Bidhaa za Matunda**

Bei ya Viazi Vitamu imeonekana kupanda katika kipindi cha wiki ya 21-27 Aprili, 2024 na 28 Aprili- 04 mei, 2024 kwa wastani wa 16.67% kutokana na kuharibika kwa miundombinu ming katika mikoa inayozalisha bidhaa hiyo kwa wingi huku bei za Muhogo na Magimbi zikibakia vile vile kutoka na kutokuwa na badiliko la mahitaji ya bidhaa hiyo.

**Bidhaa za Viungo**

Bei za viungo hazijaonesha mabadiliko yoyote ya kupanda na kushuka kutoka na sababu kuwa wafanyabiashara wakubwa wengi wa bidhaa hizo bado wana stoo ya kutosha kuweza kuleta sokoni na kulitosheleza soko bila kuathiri kiwango cha mahitaji na ugavi wa bidhaa hiyo sokoni.

**Bidhaa za Uvuvi**

Bei ya Sato imeonekana kushuka zaidi kuliko bidhaa yeyote kwa wastani wa asilimia 4.55% kutoakana kuongezeka kwa uazalishaji wa bidhaa hiyo huku bei ya Dagaa wa Nyama ikionekana kupanda zaidi kuilko bidhaa nyingine kwa wastani wa 0.91% kutokana na changamoto ya tahadhari ya uwepo wa upepo mkali wa Kimbunga cha Hidaya katika ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi.

**Bidhaa za Mifugo**

Bei za Kuku wa Kienyeji ilipanda zaidi kuliko bidhaa nyingine kwa wastani wa asilimia 12.5% kutoaka na kushuka kwa uzalishaji wa bidhaa hiyo huku bei za Mayai ya Kienyeji ilishuka zaidi kuliko bidhaa yeyote kwa wastani wa 18.28% kutokana kupungua kwa mahitaji ya bidhaa hiyo jijini Dar es Salaam.

**Bidhaa za nafaka na Kunde**

Bei za bidhaa za mtama zimeonekana kupanda zaidi ya bidaa zingine kwa wastani wa asilimia 28.74% kutokana na kuongezeka kwa mahitaji katika kipindi ambacho siyo msimu wa bidhaa hiyo katika maeneo mbalimbali nchini huku Unga wa Sembe ukionekana kushuka bei zaidi kuliko bidhaa yeyote kwa wastani wa 30.69% kutokana na kuwa msimu wa uzalishaji katika maeneo mengi nchini.

**Bidhaa za ujenzi**

Bei ya bidhaa zote za Ujenzi imeonekana kusalia vilevile katika kipindi hicho kutokana na kutokana na kuwa na kiwango sawa cha mahitaji ya bidhaa hiyo katika kipindi chote cha wiki mbili.

## 3. MAONI NA MAPENDEKEZO

3.1. Serikali iendelee kufuatilia na kutatua kero mbalimbali za kimiundombinu ya usafirishaji wa bidhaa za mazao kutoka maeneo mbalimbali ya nchi ili kuweka uwiano sawa wa viwango vya ugavi, mahitaji za bidhaa sokoni hususan katika mkoa wa Dar es Salaam;

3.2. Kuendelea kuimarisha usimamizi wa mifumo ya Taarifa za Biashara inayosimamiwa na TanTrade ili kuwa na taarifa za bei za bidhaa za mazo mbalimbali kwa wakati kutoka katika maeneo mbalimbali ya nchi, na

3.3. Wafanyabiashara wa reja reja watumie fursa za kuuza bidhaa ambazo zimeonekana kuwa na ongezeko kubwa la mahitaji kwa jamii ili kuondoa upungufu wa bidhaa hiyo sokoni. Bidhaa hizo ni pamoja na Mtama, Kuku wa Kienyeji, Samaki aina ya Sato, Viazi Viatamu, Parachichi na Vitunguu Maji.